

THE INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT



TAARIFA KWA UMMA

Jumuiya ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) pamoja na Umma kwa ujumla mnataarifiwa kuwa kuanzia mnamo mwezi Januari 2018 malipo yoyote kwa ajili ya huduma mbalimbali zitolewazo na Chuo yamekuwa yakifanyika kwa njia ya Kielektroniki kupitia mfumo ulioanzishwa na serikali ujulikanao kama Government e-Payment Gateway.

Kwa sababu hiyo, Wanafunzi pamoja na wadau mbalimbali wanatakiwa, kabla ya kufanya malipo kwa Chuo, wapate namba ya malipo (control number) kutoka kwenye mfumo wa taarifa za Mwanafunzi (Student Information System) kwa Wanafunzi ama kutoka kwenye mfumo wa malipo (Payment Portal) kwa wale wasio wanafunzi.

Namna ya Kulipa kwa Kutumia mfumo wa Kielektroniki (Government e-Payment Gateway).

Malipo kwa ajili ya Ada (Kwa Wanafunzi tu)

1. Ingia kwenye mfumo wa taarifa za mwanafunzi (**Student Information System Portal (www.ifmsis.ac.tz/studentis)**)
2. Fungua akaunti yako ya SIS
3. Bofya sehemu iliyoandikwa '**Fee Payments**' ili uweze kupata namba yako ya malipo (control number)
4. Nakiri namba yako ya malipo (control number) na kisha tembelea mojawapo ya Benki zifuatazo kwa ajili ya kulipia (**CRDB, NBC, TPB na NMB**)

Malipo Mengineyo yanayowahusu Wanafunzi

1. Ingia kwenye mfumo wa taarifa za mwanafunzi (**Student Information System Portal** (www.ifmsis.ac.tz/studentis))
2. Fungua akaunti yako ya SIS
3. Bofya Sehemu iliyoandikwa '**Other Payments**'
4. Fuata maelekezo yanayotolewa kwa ajili ya kupata namba yako ya malipo (Control number)
5. Nakiri namba yako ya malipo (Control number) na kisha tembelea mojawapo ya Benki zifuatazo kwa ajili ya kulipia (**CRDB, NBC, TPB na NMB**)

Malipo Mengineyo (kwa Wadau mbalimbali wasio Wanafunzi)

1. Ingia kweye ifmsis.ac.tz/payment_portal
2. Jaza fomu ya usajili wa malipo kwa usahihi
3. Bofya Sehemu iliyoandikwa '**Submit** bottom'
4. Subiri kwa Dakika chache
5. Bofya Sehemu iliyoandikwa '**here**' ili uweze kupata namba yako ya malipo (control number)
6. Nakiri namba yako ya malipo (control number) na kisha tembelea mojawapo ya Benki zifuatazo kwa ajili ya kulipia (**CRDB, NBC, TPB na NMB**).

Muhimu:

- Baada ya kuwasili katika mojawapo ya Benki zilizo orodheshwa, mpatie Mhudumu wa benki (teller) namba yako ya malipo (control number) pamoja na kiasi cha fedha ili aweze kukamilisha malipo hayo.
- Malipo yanaweza kufanyika kwa njia ya Mitandao ya simu za Mkononi (Tigo-Pesa, M-pesa, and Airtel Money)
 - Piga *150* 01#, au *150*00#, au *150*60# kulingana na mtandao wa simu unaotumia.
 - Chagua '**Lipia Malipo**' (**Pay Bills**)
 - Ingiza namba ya kumbukumbu ambayo ni 888999
 - Ingiza namba yako ya malipo (Control number)
 - Weka kiasi cha fedha unachotaka kulipia
 - Thibitisha muamala wa malipo kwa kuingiza neno au namba yako ya siri

Mkuu wa Chuo

Chuo ha Usimamizi wa Fedha
5 Shaaban Robert Street
S.L.P 3918

11101DAR ES SALAAM, TANZANIA

Simu: +255-22-2112931/3/4

Nukushi: +255-22-2112935

Barua Pepe: rector@ifm.ac.tz.

Tovuti: <http://www.ifm.ac.tz>